## Muhimu/Hitimisho

Udhibiti wa gummosis ni bora zaidi ukiwa wa mapema na endelevu.

Ushirikiano na wataalamu wa kilimo ni muhimu ili kutambua mapema na kuchukua hatua stahiki



Madhara ya gummosis kwenye mti wa mchungwa

TPHPA
TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY


## Wasiliana nasi:

080 011 003 1

dg@tphpa.go.tz

www.tphpa.go.tz


### Scan for More


@tphpa_tz

TPHPA TV

P.O. Box 3024 , Arusha - Tanzania
Nairobi Rd, Ngaramtoni Area


TPHPA
TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA**



# CITRUS GUMMOSIS

## UTAMBUZI

Ugonjwa unaoshambulia miti ya machungwa na kusababishwa na vimelea vya fangasi.

Ugonjwa huu hujulikana kwa kutoa utomvu mzito (gum) kwenye magome ya miti ya machungwa.

## DALILI KUU

- Kutoka kwa utomvu wa rangi ya kahawia hadi giza kwenye shina au matawi ya mti.

- Magome huvimba au kupasuka, na wakati mwingine huchubuka.

- Shina huweza kuharibika na kuonyesha madoa meupe ya kuoza.

- Majani kunyauka au kugeuka manjano.
- Mti kudhoofika au kufa taratibu.

## MADHARA

- Uharibifu wa mfumo wa usafirishaji wa virutubisho kutokana na kuoza kwa magome na shina.
- Kudhoofika kwa miti, kushindwa kuzaa au kuhimili magonjwa mengine.
- Kupungua kwa mavuno na ubora wa matunda.
- Mti unaweza kufa kabisa endapo hautatibiwa kwa wakati.




Madhara ya citrus gummosis kwenye chungwa

## UDHIBITI

### 1. Njia za kuzuia na kukinga

**Panda miti kwenye** udongo unaopitisha maji vizuri; epuka maeneo yenye maji mengi (yasiyotuama).

**Epuka majeraha kwenye magome**, kwani huweza kurahisisha fangasi kupenya

**Tumia miche yenye afya** na iliyothibitishwa kuwa haina magonjwa

**Hakikisha nafasi sahihi ya upandaji** ili kuruhusu hewa kupita.

### 2. Matumizi ya Viuatilifu.

**Ondoa magome** yaliyoathirika hadi sehemu zenye afya, kisha paka kiuatilifu kudhibi kuvu (fangasi).

**Paka kiuatilifu sehemu** zilizoathirika mara tu baada ya kupasuka au kuonekana kwa utomvu.

## TAHADHARI

- Fanya uchunguzi wa miti mara kwa mara.
- Tumia mbolea kwa usahihi ili mti uwe na kinga nzuri.
- Okoa miti kwa kuzuia kuenea kwa ugonjwa kwa kupogoa matawi yaliyoathirika.



Madhara ya citrus gummosis kwenye tunda